# HALMASHAURI YA WILAYA KONDOA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)


WILAYA YA K0NDOA
Fax/Simu 026 2360313
E-Mail: ded@kondoadc.go.tz

S.L.P. 1
KONDOA.


KUMB. Na: KDC/R10/2VOL.II/46

15/06/2017

# TANGAZO

## ILANI YA KUSUDIO LA KUTUNGA SHERIA NDOGO SHERIA NDOGO (KUZUIA UPOTEVU NA UHARIBIFU WA NAFAKA WAKATI NA BAADA YA KUVUNA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KONDOA ZA MWAKA 2017

**(Chini ya Kifungu cha 155(1) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) [Sura ya 287, Toleo la Mwaka, 2002])**

Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa inawatangazia Wananchi wote ambao ni wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa kuwa inakusudia kutunga Sheria Ndogo (Kuzuia Upotevu na Uharibifu wa Nafaka wakati na baada ya Kuvuna) za Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa za Mwaka 2017 kwa mujibu wa mamlaka iliyopewa chini ya kifungu cha 153 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) [Sura ya 287, Toleo la Mwaka, 2002] na Sheria zingine za Nchi.

**Lengo la Sheria ndogo hizi ni:**

1. Kudhititi upotevu na uharibifu wa mazao ya nafaka kabla na baada ya mavuno
2. Kuzuia magonjwa ya mazao ya nafaka yanayotokana na njia mbovu za uvunaji, upukuchuaji na uhifadhi,
3. Kudhibiti matumizi mabaya ya viuatilifu,
4. Pia zitaweka udhibiti wa vipimo vya ujazo.

Wananchi wote ambao ni wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya kondoa, mnaombwa kushiriki katika kutunga Sheria hizi kwa kutoa maoni kukubaliana nazo au kutoa pingamizi au hoja za kupinga. Rasimu ya sheria ndogo hizi imewekwa/ inapatikana kwenye Ofisi za maafisa watendaji wa kata na vijiji vyote vya Halmashauri (w) Kondoa, Mkurugenzi Mtendaji(W) Kondoa na ofisi ya Mwanasheria (W) Kondoa .

Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa inawataarifu Wanachi wote ambao ni wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa kwamba, pingamizi au hoja zozote kuhusu rasimu ya sheria ndogo hizi ziwasilishwe kwa Maandishi katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa au kwa S.L.P 1 Kondoa kabla ya tarehe **15, Julai, 2017.**

**LIMETOLEWA NA MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KONDOA**
**S.L.P 1**
**KONDOA**

MWL. FALESY MOHAMED KIBASSA
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**KONDOA**

MKURUGENZI MTENDAJI WA WILAYA
KONDOA

Tangazo la Serikali na........................ la Tarehe..........................

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA YA WILAYA)

(SURA 287)

---

SHERIA NDOGO.

---

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 153 (1)*

---

# SHERIA NDOGO (KUZUIA UPOTEVU NA UHARIBIFU WA NAFAKA WAKATI NA BAADA YA KUVUNA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KONDOA ZA MWAKA 2017

## SEHEMU YA KWANZA
## UTANGULIZI

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo (Kuzuia Upotevu na Uharibifu wa Nafaka wakati na baada ya Kuvuna) za Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa za Mwaka 2017 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa

Tafsiri

3. Katika Sheria ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Afisa ugani" Maana yake ni Afisa mwenye dhamana ya masuala ya mifugo, Kilimo na chakula kuanzia ngazi ya Wilaya hadi Kijiji;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa

"Matumizi mabaya ya chakula" Maana yake ni matumizi ambayo yanaweza kusababisha upungufu au uhaba wa chakula katika eneo au kaya husika na ambayo hayahusiani na matumizi ya chakula;

"Mazao ya chakula" Maana yake ni mazao ambayo hutumika kwa chakula cha binadamu;

"Mkulima" maana yake ni mtu yeyote anayejihusisha na shughuli za kilimo cha mazao ya nafaka;

"Mkurugenzi" Maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa pamoja na Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Nafaka" maana yake ni mazao yafuatayo; Mahindi, Mpunga, Uwele, Ufuta, Mtama, Ngano, Shayiri, jamii ya mikunde, na alizeti;

"Ubora wa Nafaka" maana yake ni hali ya kudumisha uhalisia wa ukubwa wa punje, usafi, uzito na usalama wa nafaka kwa kuzingatia taratibu za kilimo bora;

"Uhifadhi" maana yake ni utaratibu bora wa kutunza nafaka katika sehemu ambayo haitasababisha upotevu na uharibifu wa nafaka;

"Ukaushaji" maana yake ni taratibu sahihi za kukausha nafaka kwa ajili ya matumizi au kuhifadhi;

"Upepetaji" maana yake ni mbinu sahihi za kuondoa uchafu katika nafaka;

"Upotevu wa nafaka" maana yake ni kushindwa kupata na kutunza kiasi chote cha nafaka inayovunwa;

"Usafirishaji" maana yake ni taratibu zinazotumika kusafirisha nafaka kutoka shambani kwenda eneo la kupukuchulia, au eneo la kukaushia, au kuhifadhia, au kutoka shambani kwenda sokoni, au kutoka eneo la kuhifadhia kwenda sokoni;

"Uvunaji wa nafaka" maana yake ni uvunaji wa mazao ya nafaka baada ya kukomaa na au kukauka;

"Vipimo vya nafaka" maana yake ni vipimo vilivyoelekezwa na Wakala wa Vipimo wa Serikali kutumika katika kupima nafaka ikiwa ni pamoja na mizani;

"Viuatilifu"maana yake ni sumu ya kuua au kuzuia wadudu waharibifu wa nafaka;

"Viumbe waharibifu" maana yake ni wanyama, ndege au wadudu ambao huharibu mimea au mazao ya chakula shambani au ghalani;

"Wakala wa Vipimo wa Serikali" kama ilivyoanzishwa na Sheria ya Sura ya 245 ya Mwaka 2002;

"Waziri" Maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

## SEHEMU YA PILI
## UVUNAJI, UPUKUCHUAJI, UKAUSHAJI, USAFIRISHAJI NA UHIFADHI WA NAFAKA

Wajibu wa kuzingatia taratibu za uvunaji

4. Kila mkulima atakuwa na wajibu wa kuzingatia taratibu za uvunaji bora wa nafaka zilizowekwa na Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa kuvuna.

5. -(1) Kila mkulima atakuwa na Wajibu wa-

(a) Kufuata ratiba za uvunaji wa mazao kwa wakati baada ya mazao kukomaa;

(b) Kuvuna nafaka kwa kuzingatia njia sahihi zisizosababisha uharibifu, upotevu na kupungua kwa ubora wa nafaka zitakazoelekezwa na Halmashauri;

(c) Kutumia njia sahihi za upukuchuaji au upuraji wa nafaka ambazo hazisababishi uharibifu na upotevu wa nafaka;

(d) Kutoa taarifa kwa Afisa ugani kuhusu uwepo wa tatizo lolote katika nafaka;

(e) Kushiriki mafunzo ya njia bora za uvunaji wa nafaka na kutekeleza ujuzi uliopatikana kwenye mafunzo hayo.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 5 (1)(b) na (c) njia sahihi za uvunaji na upukuchuaji wa nafaka ni pamoja na zisizoacha nafaka shambani na zisizoharibu nafaka.

Wajibu wa Halmashauri

6. -(1) Halmashauri itakuwa na wajibu wa-

(a) kutoa elimu ya mbinu bora za uvunaji ili kutoharibu, na kupoteza nafaka;

(b) kuhakikisha angalau kila kata inakuwa na Afisa Ugani Mmoja;

(c) kuhakikisha upatikanaji rahisi na kwa wakati wa pembejeo za kilimo na viuatilifu;

(d) Kuhamasisha uanzishwaji wa Vituo vya kukusanyia Nafaka na masoko;

(e) kuanzisha mashamba darasa na vituo maalum kwa ajili ya kutolea mafunzo ya utumiaji wa zana bora za kilimo na uvunaji bora usioharibu, kupoteza au kupunguza ubora wa nafaka;

(f) Kusimamia biashara ya Mazao ya Nafaka kwa kuhakikisha upatikanaji wa soko, na utumiaji wa vipimo elekezi;

(g) kusimamia upatikanaji, maadili na mwenendo wa mawakala wa mbolea, pembejeo za kilimo na viuatilifu;

(h) kuhamasisha Serikali za vijiji na wananchi kwa ujumla kujenga maghala ya chakula ya vijiji;

(i) kuhakikisha viongozi wa Serikali, vyama vya siasa na wadau wengine wanashiriki ipasavyo katika kuendeleza sekta ya kilimo katika Halmashauri;

(j) kuhamasisha uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika;

(k) Kufanya ufuatiliaji wa uwasilishwaji wa taarifa za maendeleo ya kilimo na uvunaji bora kutoka katika ngazi za Kijiji, Kata, na Tarafa;

Usafirishaji wa nafaka

7. -(1)Kila mkulima anawajibu wa kutumia njia sahihi za usafirishaji wa nafaka ambazo hazisababishi uharibifu na upotevu;

(2) Mkulima atawajibika kusafirisha nafaka kwa kutumia njia bora za asili na kisasa ambazo hazisababishi upotevu na uharibifu wa nafaka;

(3) Endapo Mkulima atatumia tela au mkokoteni wa aina yoyote atatakiwa kuhakikisha kuwa tela hilo au mkokoteni huo umefunikwa, hauna unyevunyevu, au hauna nyufa zinazoweza kusababisha upotevu wa nafaka.

Kukausha nafaka

8. -(1)Kila Mkulima atatakiwa kukausha nafaka kwa kutumia njia sahihi zitakazoelekezwa na Afisa Ugani ambazo hazitasababisha uharibifu na upotevu wa nafaka baada ya kuvuna.

(2) Njia sahihi za ukaushaji wa nafaka ni pamoja na-

(a) Kuandaa mazingira safi ya kukaushia au kuanikia nafaka;
(b) Kuanika kwa njia ya asili kwa kutumia jua;
(c) Kuanika juu ya vitambaa safi, mikeka ya aina mbalimbali, vichanja vinavyozuia upotevu na kuharibu ubora wa nafaka; na
(d) Kuanika kwa njia nyingine yeyote sahihi inayopendekezwa na Afisa Ugani.

Ukaushaji wa nafaka usiofaa

9. Ni marufuku kukausha nafaka kwa kutumia njia zisizo sahihi zinazosababisha uharibifu, upotevu na kupunguza ubora wa nafaka ambazo ni-

(a) Kuanika chini kwenye udongo, vumbi au mchanga;

(b) Kukausha nafaka ambazo hazijakomaa;

(c) Kukausha nafaka kwa kutumia moshi au vifaa visivyofaa;

(d) Kukausha nafaka katika mazingira yasiyo salama na yasiyoandaliwa kwa lengo la kukaushia nafaka.

Usafi wa nafaka

10. -(1) Nafaka zitasafishwa kwa kutumia vifaa safi na salama ambavyo vitazuia;

(a) upotevu,
(b) uharibifu na
(c) kupunguza ubora wa nafaka.

(2) Nafaka zinaweza kusafishwa kwa Kuchambua, kupepeta na kuchekecha kwa nia ya kutenganisha au kuondoa uchafu, makapi, vumbi na vitu vingine ambavyo

si nafaka husika.

Uhifadhi wa nafaka

11. -(1) Mkulima atawajibika kuhifadhi nafaka katika vifaa maalum kwa kutumia njia sahihi za kiasili na za kisasa ambazo hazitasababisha uharibifu, upotevu na kupunguza ubora wa nafaka.

(2) Njia sahihi zinazoelekezwa kutumika kuhifadhi nafaka ni pamoja na-

(a) Magunia yenye kiwambo yasiyopitisha hewa;
(b) Magunia ya kawaida kwa ajili ya nafaka zilizowekwa viuatilifu;
(c) Kihenge bora cha asili;
(d) Silo au pipa maalum;
(e) Ghala bora lililo safi; na
(f) Kutumia viuatilifu kwenye nafaka kwa kuzingatia ushauri wa kitaalam;

(3) Ghala au vyombo vilivyosafishwa kwa viuatilifu vya majimaji vitatumika baada ya kukauka.

Wajibu wa kutoa taarifa

12. -(1)Mkulima atakuwa na wajibu wa kutoa taarifa kwa Afisa Mwidhiniwa kuhusu uwepo wa wadudu au wanyama waharibifu au Mtu yeyote atakayetenda jambo litakolosababisha uharibifu, upotevu na kupunguza ubora wa nafaka.

(2) Ni wajibu wa kila Mkulima kuzingatia na kufuata ushauri wa kitaalam.

(3) Ni wajibu wa Mkulima kukagua ghala au sehemu anayohifadhia nafaka mara kwa mara.

Matumizi ya viuatilifu

13. -(1) Halmashauri itakuwa na wajibu wa kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa pembejeo na viuatilifu kwa ajili ya kuhifadhia nafaka;

(2) Mkulima atatumia viuatilifu kwa namna atakavyoelekezwa na Afisa Ugani;

(3) Wauzaji na wasambazaji wa pembejeo na viuatilifu vya kuhifadhi nafaka watawajibika kusambaza kwa Wakulima pembejeo na viuatilifu vilivyosajiliwa na vyenye ubora unaostahili.

(4) Kabla ya kutumia viuatilifu, Mkulima atahakikisha kuwa nafaka zimekauka vizuri, zimesafishwa na kutenganishwa na uchafu wa aina yoyote.

Viuatilifu vya majimaji

14. -(1) Viuatilifu vya maji maji vitatumika kuoshea ghala au vyombo vingine vya kuhifadhia nafaka kabla ya kuweka nafaka kwa ajili ya kuua wadudu na kinga.

(2) Ni marufuku kutumia viuatilifu vya aina ya maji maji kwenye nafaka isipokuwa kwa maelekezo ya Afisa Ugani.

Vipimo vya nafaka

15. -(1) Nafaka zitauzwa kwa kipimo cha Kilo au kipimo chochote kinachotambuliwa na Wakala wa Vipimo wa Serikali;

(2) Ni marufuku kuuza nafaka kwa kutumia vipimo vya ujazo ambavyo ni

Gunia, Kiroba, Debe, Ndoo, Visado au vifaa vingine vya ujazo au Lumbesa.

Marufuku

16. Ni marufuku kwa Mkulima yeyote-

(a) Kuvuna, kupukuchua, kusafirisha, kukausha, kusafisha na kuhifadhi nafaka kwa kutumia njia zisizo sahihi ambazo zitasababisha uharibifu, upotevu na kupunguza ubora wa nafaka;

(b) Kuuza mazao shambani au sehemu nyingine yoyote ambayo si sehemu ya kukusanyia mazao ya nafaka au soko;

(c) Kutumia viuatilifu visivyoruhusiwa, vilivyopitwa na wakati wa matumizi, bandia, au kutumia viuatilifu bila maelekezo ya Afisa Ugani;

(d) Kuhifadhi au kusafirisha nafaka kwenye vifaa ambavyo awali vilitumika katika kuhifadhi au kusafirisha vitu ambavyo ni hatari kwa afya ya Binadamu;

Makosa na adhabu

17. -Itakuwa ni kosa chini ya Sheria Ndogo hizi kwa Mtu yeyote-

(a) Atashindwa kuvuna mazao yaliyoko shambani ambayo yamefikia wakati wa kuvunwa;
(b) Atakuwa na ghala la kuhifadhia mazao na kushindwa kulitumia;
(c) kutohifadhi chakula cha kutosha;
(d) kuuza mazao bila kuweka akiba ya mwaka mzima au zaidi;
(e) kuuza mazao yakiwa shambani kwa Walanguzi;
(f) kuuza mahindi mabichi isipokuwa kama Mkulima alitoa taarifa kwa Mamlaka husiku kuwa Shamba hilo limeandaliwa kwa ajili ya biashara ya Mahindi mabichi;
(g) kutumia vibaya viuatilifu;
(h) au kutenda jambo lolote lililokatazwa na Sheria Ndogo hizi.

Adhabu

Mtu yeyote atakayetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi Laki tatu (300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili (12) jela au adhabu zote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hii kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri ulioitishwa na kufanyika tarehe ..................................2017 na kushuhudiwa na:-

..............................................

MWL. FALESY MOHAMED KIBASSA,
**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa.**

..............................................

HIJA SURU,
**Makamu Mwenyekiti,**
**Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa**

**NAKUBALI**

..............................................

GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB.)
**Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI**

DODOMA
………………./……………/2017